



## BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

### ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

#### BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

#### MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 28 Februari, 2025.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua itasomwa.

#### I. TAARIFA YA SPIKA:

#### II. MASWALI:

##### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

185. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Katika juhudi za kuwasaidia wakulima katika ukanda wa mashariki ya Pemba, Serikali ilijenga matuta ya kuzuia maji chumvi likiwemo tuta la Tovuni katika shehia za Kiungoni na Mjananza. Hata hivyo, baada ya muda mfupi tu tuta la Tovuni limeharibika vibaya sana na kusababisha maji kuja na sehemu ya tuta kufukuka.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulitunza tuta hilo.
- (b) Je, ni lini Serikali italifanya marekebisho tuta hilo ili liendelee kuwasaidia wakulima wa mashamba ya kilimo cha juu yaliyopo katika shehia za Kiungoni na Mjananza.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

78. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Watumishi wanaoelekea kustaafu ni muhimu sana kupatiwa elimu ya kuishi baada ya utumishi wao.

Je, Serikali imefanya tathmini ipi ya kuhakikisha kuwa mafunzo hayo yanafikia lengo lililokusudiwa.

102. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudini kubwa inayochukua ya kujenga majengo mapya ya Mahakama.

Je, ni kwa kiasi gani mageuzi mbali mbali yaliyofanyika kwenye Mahakama zetu yanarahisisha upatikanaji wa haki.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

71. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi na utawala Bora:

Kumejitozea changamoto ya ufungaji wa mikataba ya kisheria baina ya wawekezaji wa kigeni na wananchi wa jimbo la Paje, kiasi ya kupelekea kudhulumiwa haki zao.

- (a) Je, Wizara yako ina ufahamu wowote wa changamoto hii.
- (b) Ni lini Wizara yako itawapatia wananchi wa jimbo la Paje, mwanasheria wa kutoa elimu katika jimbo hilo.
- (c) Je, unawaeleza nini wananchi waliopata changamoto hiyo ya kudhulumiwa haki zao.

### Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

91. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa Zanzibar ni nchi ya visiwa inayotegemea sana kuimarika kwa mawasiliano ya mtandao wa intaneti ili kuwasiliana na dunia na kukuza uchumi wake, hasa katika kipindi hiki tunaposhuhudia uwekezaji mkubwa katika sekta ya utalii na miradi mikubwa ya kimkakati nchi nzima.

Je, ni lini Wizara yako itahakikisha kuwa nchi yetu inakuwa na mfumo imara wa huduma vumilivu wa mtandao wa internet kwa nchi nzima ili kukuza biashara na uchumi wa Zanzibar.

### Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

113. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Mikakati ya kuwaendeleza vijana katika tasnia ya ubunifu inachukua sura gani kwa sasa.

### Wizara ya Afya:

125. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa tumeshuhudia ujenzi wa hospitali nyingi za Wilaya na Mkoa umekamilika kwa kiwango cha ubora.

Ni lini suala la ujenzi wa nyumba za makaazi za madaktari litapewa kipaumbele kinachostahili.

138. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Tathmini ya uwiano wa wagonjwa na wahudumu wa afya iko viperi kwa sasa.

- (b) Kwa kiasi gani tathmini hiyo inachochea ustawii bora  
katika kupatikana huduma za afya.

Zanzibar,  
28 Februari, 2025.



(Raya Issa Msellem)  
KATIBU WA BARAZA.